BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Saba – Tarehe 23 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

193. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Je, kuna tafiti yoyote ya hivi karibuni inayotoa tathmini halisi ya ukataji wa miti na uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa mchanga na vifusi hapa Zanzibar.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kiasi gani vikosi vyetu vya SMZ vina uwezo wa kutosha katika matumizi ya zana za majanga tofauti ikiwemo ajali za baharini.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

92. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ilichagua kutumia mfumo wa kununua magari ya Serikali kwa pamoja (Bulk Procurement System) kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa lengo la kuongeza ufanisi na kupunguza gharama ya ununuzi kwa Serikali. Licha ya matarajio ya kuwa mfumo huu ungeleta unafuu na ufumbuzi katika manunuzi hayo, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa taasisi za umma, hasa kuhusu ucheweleshaji wa magari hayo.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hutumika kununulia magari hayo kwa mwaka tokea kuanza kwa mfumo huu.

(b) Je, ni taasisi ngapi zimeshapatiwa magari na ni taasisi zipi ambazo bado zinasubiri magari yao.

(c) Je, ni sababu zipi zinazosababisha kucheleweshwa kwa ununuzi wa magari kupitia mfumo huu na ni mkakati gani wa Serikali unaotekelezwa kuondoa mkwamo huu.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

178. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Wajasiriamali wengi wana changamoto ya kupata masoko.

(a) Ni kwa kiasi gani na kwa njia zipi Wizara yako inazitumia katika kuwapa wajasiriamali wetu elimu ya masoko kwa njia ya kimtandao (Digital Marketing).

(b) Ni wajasiriamali wangapi na kwa vipi wameweza kufanikiwa kupata elimu hii ili kuweza kuwa kigezo na msaada kwa wajasiriamali wenzao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

260. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Msingi ya Mchanga Mdogo imekumbwa na matatizo sugu ya uchakavu wa majengo yake, ikiwa ni pamoja na kuvujisha, nyufa zake kuwa kubwa na hatarishi kiasi ambacho imepoteza sifa ya kuwa eneo la kufundishia na kujifunzia.

(a) Vipi Serikali yetu inalitambua tatizo hilo.

(b) Ni hatua gani za dharura na za muda mrefu zinazochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

187. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni kwa namna gani kiswahili, uswahili, mswahili, waswahili, uswahilini, na asili ya mzizi swahili vimekuwa vivutio vya utalii nchini.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

147. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na malalamiko juu ya ujazo wa magari yanayofanya biashara ya kubeba mchanga Zanzibar, kwamba yanafanya biashara ya kubeba mchanga bila ya kupimwa ujazo wake na mamlaka zinazohusika na vipimo

(a) Je, ni mamlaka gani yenye wajibu wa kuhakikisha kuwa magari haya yanapimwa ipasavyo.

(b) Je, ni taasisi gani yenye wajibu wa kusimamia mapato ya shughuli hii hapa Zanzibar.

(c) Je, ni magari mangapi yanayofanya biashara hii hapa Zanzibar na ni kiasi gani cha mapato yameingia Serikalini kwa mwaka 2023.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

170. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini ikoje kwa sasa juu ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini, ili tuweze kujitegemea na kupunguza utegemezi wa mazao ya chakula kutoka nchi jirani na nchi za nje.

181. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini ya kuimarika na changamoto za kilimo hai ziko vipi kwa sasa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini**

91. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusu usahihi wa mita za umeme zinazofungwa na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO). Wananchi hao hulalamikia usahihi katika vipimo na ubora wa mita hizo, pamoja na usalama wa watumiaji.

(a) Je, Serikali inatumia mbinu gani kuhakikisha ubora na usalama wa mita za umeme kabla ya kufungwa kwa mtumiaji wa mwisho.

(b) Je, ni mita ngapi za umeme zinazoingizwa kila mwaka na mapato yanayokusanywa na ZECO ni kiasi gani.

(c) Je, ni kwa namna gani Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) wanashirikishwa katika upimaji wa mita hizi zinazoingizwa Zanzibar.

**Wizara ya Afya:**

13. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha afya cha Kiembesamaki kinatoa huduma za afya kwa shehia zaidi ya nne na wadi zaidi ya mbili. Hata hivyo, kituo hicho kipo katika hali mbaya sana na hatarishi, pamoja na viongozi wa Wizara hii kutoa ahadi mara kadhaa ya kukikarabati kituo hicho bila ya kuzitekeleza ahadi zao hadi leo hii.

Je, ni lini Wizara yako itaitekeleza ahadi yake ya kukikarabati kituo hicho.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

240. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi B amekuwa akilisimamia na kulipigania suala la upotevu wa mianya ya mapato kupitia bandari bubu.

Ni kwa kiasi gani Shirika la Bandari la Zanzibar linatoa mchango stahiki katika mapambano haya kwa kuweka wasimamizi wa kutosha hususani kwenye maeneo ya Kisakasaka, Fumba na Bweleo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**23 Mei, 2024.** **KATIBU WA BARAZA**